



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA WILAYA YA IRAMBA

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na DED/IRA/S.10/5/Vol. III/21

23 Mei 2022.

TANGAZO LA KAZI

MKURUGENZI MTENDAJI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA IRAMBA
ANAKARIBISHA MAOMBI YA KAZI KWA WANANCHI WOTE WENYE
SIFA ZA KUJAZA NAFASI ZIFUATAZO

Kwa mamlaka aliyopewa chini ya Sheria ya Utumishi wa Umma na marekebisho yake Na. 8 ya mwaka 2014, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Iramba anawatangazia watanzania wote nafasi za ajira zifuatazo:

1. MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III - NAFASI 13

a) Sifa za Mwombaji

Mwenye Elimu ya kidato cha nne (IV) au sita (VI); aliyehitimu Mafunzo ya Astashahada/cheti katika moja ya fani zifuatazo. Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa fedha, Maendeleo ya jamii na Sanyansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali. Astashahada yenye alama ya NTL. Level 5 (Basic Technician)

b) Kazi na Majukumu

- Afisa masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali za Kijiji
- Kusimamia ulinzi na usalama wa raia na Mali zao, kuwa mlinzi wa amani na msimamizi wa Utawala bora katika Kijiji.
- Katibu wa Mikutano na kamati za Halmashauri ya Kijiji
- Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria, taratibu, Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma.
- Kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza Mikakati ya kuondoa njaa, umasikini na kuongeza uzalishaji mali.
- Kiongozi wa wakuu wa vitengo vya Kitaalam katika Kijiji
- Kusimamia kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za Kijiji.
- Mwenyekiti wa Kikao cha wataalamu waliopo katika Kijiji

- Kupokea, kusikiliza na kutatua malalamiko na Migogoro ya Wananchi
- Kusimamia utungaji wa Sheria ndogo za Kijiji.
- Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata.
- Ngazi ya mshahara TGS B.

2. KATIBU MAHSUSI DARAJA LA III - NAFASI 3

(a) Sifa za Mwombaji

- Wahitimu wa kidato cha nne (IV) aliyehudhuria mafunzo ya uhazili na kufaulu mtihani wa hatua ya tatu. (Basic Technician NTL Level 5).
- Wawe wamefaulu somo la hati mkato ya Kiswahili na Kiingereza maneno 80 kwa dakika moja na wawe wamepata mafunzo ya kompyuta kutoka chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali na kupata cheti katika program za Windows, Microsoft Office, Internet, E – mail na Publisher.

(b) Kazi na Majukumu

- Kuchapa barua, taarifa, na nyaraka za kawaida
- Kusaidia kupokea wageni na kuwasaili shida zao na kuwaelekeza sehemu wanazoweza kushughulikiwa.
- Kusaidia kutunza taarifa/kumbukumbu za matukio, miadi, wageni, tarehe za vikao.
- Kusaidia kutafuta na kumpatia Mkuu wake majalada, nyaraka au kitu chochote kinachohitajika katika shughuli za ofisi.
- Kusaidia kupokea majalada, kuyagawa kwa maofisa walio katika sehemu alipo.
- Kutekeleza kazi zozote atakazopangiwa na msimamizi wake wa kazi
- Ngazi ya mshahara TGS B.

3. MAELEZO YA JUMLA

a) Sifa za Mwombaji

- Awe Mtanzania.
- Awe hajawahi kufungwa, kupunguzwa au kufukuzwa kazi Serikalini.
- Awe na umri wa kuanzia miaka 18 hadi 45.
- Awe mwenye akili timamu.

b) Mambo ya Kuzingatiwa

- Barua ya maombi iambatishwe na nakala za Vyeti vya taaluma na Cheti cha kuzaliwa vikiwa vimethibitishwa kisheria. Pia waambatishe: Picha za rangi mbili (2) za "passport size" za hivi karibuni; Maelezo binafsi (CV) yakionesha anuani kamili, wadhamini watatu, na namba ya simu ya mkononi, itakayo kuwa rasmi kwa mawasiliano; na Namba ya utambulisho wa utaifa (Namba ya NIDA).
- Waombaji waliosoma nje ya nchi waambatishe uthibitisho kutoka baraza la Mitihani Tanzania (NECTA) na/au Baraza la Elimu ya Ufundi Tanzania (NACTE).
- Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **06 Juni 2022**.
- Watakao kuwa wamekidhi vigezo vya kuitwa kwenye ushahidi watajulishwa.

- Maombi yote yatumwe kwa njia ya posta tu, kwa anwani ifuatayo:

**Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Iramba,
S. L. P. 155,
Kiomboi – IRAMBA.**

Tangazo hili limetolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya.



**Michael A. Matomora
MKURUGENZI MTENDAJI**

23 Mei 2022

**MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA IRAMBA**